EQUATOR INITIATIVE

UNDP

*Empowered lives.*
*Resilient nations.*




# HIFADHI YA ASILI YA AMANI

Tanzania


## Miradi ya Equator

Wanafijiji na Maendeleo Himili ya Jamii

# MIRADI YA UNDP EQUATOR

Kote duniani, jamiii zinazidi kubuni mbinu zinazonuiwa kuyakidhi mahitaji yao ya kila siku na ya kimazingira. Kuna kazi chache ambazo zimechapishwa za kuelezea kinagaubaga hizo mbinu bunifu na vile zilianzishwa,vile ziliathiri wakaaji wa sehemu mbali mbali na vile zimekuwa zikibadilika pindi wakati unapotita. Wachache wamejitokeza kuelezea wazi wazi juu ya miradi yao, na hata wale ambao wamefanya hivyo ni wakuu wa vijiji ambao wamefanya kuelezea kufaulu kwao.

Mradi huu wa Equator Katika unadhamiria kujaza hili pengo kama njia moja ya kuadhimisha miaka kumi tangu kuanzishwa kwake. Masimulizi juu ya huu mradi ni baadhi tu ya mingi ambayo imefaulu na kushinda tuzo za Equator baada ya kukaguliwa na kutathiminiwa katika kitengo cha makundi ya kijamii yanayo hifadhi mazingira na kuinua maisha ya wanafijiji. Miradi hii inakusudiwa kuwa mifano ya kuiwa na kuwatia shime kuzungumzia ilivyofaulu ili kuhamasisha ulimwengu juu ya uhifadhi wa mazingira.



*Bonyeza katika ramani ya miradi ya Equator ili upate kupata habari zaidi.*


### Wahariri

| | |
|---|---|
| *Mhariri Mkuu :* | Joseph Corcoran |
| *Muhariri Meneja :* | Oliver Hughes |
| *Wahariri Waliochangia :* | Dearbhla Keegan, Matthew Konsa, Erin Lewis, Whitney Wilding |

### Wahandishi Waliochangia

Edayatu Abieodun Lamptey, Erin Atwell, Toni Blackman, Jonathan Clay, Joseph Corcoran, Larissa Currado, Sarah Gordon, Oliver Hughes, Wen-Juan Jiang, Sonal Kanabar, Dearbhla Keegan, Matthew Konsa, Rachael Lader, Patrick Lee, Erin Lewis, Jona Liebl, Mengning Ma, Mary McGraw, Gabriele Orlandi, Brandon Payne, Juliana Quaresma, Peter Schecter, Martin Sommerschuh, Whitney Wilding, Luna Wu

### Uchoraji

Oliver Hughes, Dearbhla Keegan, Matthew Konsa, Amy Korngiebel, Kimberly Koserowski, Erin Lewis, John Mulqueen, Lorena de la Parra, Brandon Payne, Mariajosé Satizábal G.

### Shukrani

Equator ingependa kuwashukuru wanachama wa Hifadhi ya Asili ya Amani na haswa mwongozo na mchango wa Stephen Mmasi na Godfrey Msumari. Picha ni za Hifadhi ya Asili ya Amani, ramani ni za CIA World Factbook na Wikipedia.

### Nukuu Ziada

United Nations Development Programme. 2012. *Hifadhi ya Asili ya Amani, Tanzania*. Equator Initiative Case Study Series. New York, NY.

# HIFADHI YA ASILI YA AMANI
## Tanzania

### MUHTASARI WA MRADI

Hifadhi ya Asili ya Amani ilianzishwa ili kulinda mfumo wa kipekee wa ikolojia ya Mashariki mwa Milima ya Usambara iliyopo Mashariki mwa Tanzania. Hifadhi hii ya viumbe hai inachukua eneo lenye hekta 83,600 na ni makazi ya binadamu na spishi nyingine za kipekee zisizopatikana mahali pengine popote duniani. Jamii zimejihusisha katika usimamizi wa hifadhi hii tangu ilipoanziashwa mwaka 1997. Wawakilishi wawili wa jamii ni wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Hifadhi ya Asili ya Amani.

Utegemezi mkubwa wa jamii za kijadi katika maliasili zilizopo katika eneo hili kilikuwa ndicho kikwazo kikubwa katika kulifikia lengo la kuhifadhi msitu wa kipekee wa Amani. Bodi ya Usimamizi wa Hifadhi imeanzisha jitihada inayolenga kuanzisha matumizi yasiyo ya ulaji wa maliasili hii na shughuli za kujiongezea kipato kama vile utalii wa mazingira, ufugaji wa nyuki samaki na vipepeo.

### MUHTASARI


MSHINDI WA TUZO YA EQUATOR: 2006

ULIANZISHWA: 1997

ENEO: East Usambara Mountains

WANAOFAIDI: Over 400 community members employed

MAZINGIRA: 83,600-ha Amani Nature Reserve



### YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Historia na Mandhari | 4 |
| Majukumu Makuu na Ubunifu | 6 |
| Matokeo ya Kimazingira | 7 |
| Matokeo ya Kijamii | 8 |
| Matokeo ya Kisera | 9 |
| Jinsi ya Kudumisha Mradi Huu | 10 |
| Maono | 10 |
| Wahisani | 10 |

# **Historia** na Mandhari



Hifadhi ya Asili ya Amani ilitangazwa kisheria na Serikali ya Tanzania katika gazeti la serikali mwaka 1997, ikiwa na lengo la kuihifadhi bayoanuwai ya Milima ya Usamabara Mashariki. Safu ya Mashariki ya Milima ya Usambara imeorodheshwa kama kituo cha kimataifa cha bayoanuwai ya mimea na inajivunia kuwa ya pili kwa kuwa na aina nyingi za mimea katika bara la  Afrika. Pia ilitangazwa na UNESCO kuwa Hifadhi ya Binadamu na Viumbe hai, mwaka 2000. Hifadhi hii ya viumbe hai yenye eneo la takribani hekta 83,600 inajumuisha misitu ya mvua na ardhi ya nyasi na miti ya uwanda wa chini. Ina sifa ya kuwa na mimea mingi iliyo katika hatari ya kutoweka (ikiwemo mimea mingi ya madawa) na ni makazi ya zaidi ya aina kumi na tatu za ndege wasiopatikana mahali pengine. Pia misitu hii mikuu hutoa maji kwa wakazi zaidi ya 300,000 katika mji wa Tanga, na wenyeji wa milimani wanategemea misitu hii kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimaisha.

## *Kuhifadhi masalia ya mwisho ya msitu wa mvua*

Mifumo ya ikolojia ya Usambara Mashariki iliharibiwa vibaya kuanzia miaka ya 1950 na kuendelea, kutokana na ukataji mkubwa wa miti uliokuwa ukifanywa na makampuni ya kigeni. Kiwanda cha mbao kilianzishwa Tanga kwa ajili ya usindikaji wa miti ya Usambara na kutengeneza mbao nyembamba na kupanua kazi zake miaka ya 1970 kwa ufadhili wa shirika la maendeleo la Ufini. Baada ya kuupunguza msitu kwa kiasi kikubwa kutokana na uwekezaji wao katika Mradi wa Msitu wa Eneo la Mkusanyiko wa Maji Mashariki mwa Usambara (EUCFP), miaka ya 1990, Ufini iligeuka na kuanza kulihifadhi eneo la mkusanyiko wa maji, viumbe hai walio hatarini kutoweka na kuendeleza huduma za mfumo wa ikolojia kwa ajili ya jamii za wenyeji. Uanzishwaji wa hifadhi za misitu za taifa ulionekana kuwa mbinu bora zaidi ya uhifadhi, na kati ya mwaka 1991 na 1998, jumla ya dola za kimarekani milioni 6.1 zilitumika ili kulifikia lengo hili. Kituo cha Sheria za Mazingira cha IUCN kilichukua jukumu la kiushauri, kwa kueleza masuala mbalimbali ya kisheria kuhusiana na hifadhi. Mchakato wa utafiti na uchoraji wa ramani vilikamilika mwaka 1994; na ndipo Hifadhi ya Asili ya Amani ikaanzishwa mwaka 1997. Hifadhi hii iliundwa na hifadhi sita za misitu ambazo ni Kwamkoro, Kwamsambia, Mnyuzi Scarp, Amani Zigi, Amani Mashariki na Amani Magharibi zikiwa na jumla ya hekta 8,380. Hii inajumuisha hekta 1,065 zinazomilikiwa na makampuni binafsi ya chai chini ya usimamizi wa Kampuni ya Chai ya Usambara Mashariki. Inajumuisha pia Bustani ya Mimea ya Amani iliyoanzishwa mwaka 1902 chini ya utawala wa kikoloni na bado ni moja ya bustani kubwa kabisa za mimea Afrika. Hifadhi hii imeendelezwa kama kituo cha utalii, kikiwa na hoteli mbili na njia za kupita msituni, na pia kimekuwa kivutio kikubwa kwa watafiti wa ndani na nje.

Hifadhi ya Asili ya Amani ina aina kuu mbili za misitu. Katika uwanda wa chini, kuna misitu ya miti inayopukutisha majani ambayo inapata mvua kidogo, na inachukua theluthi ya eneo la hifadhi. Misitu ya kijani iliyopo chini ya milima inapata mvua kwa wingi na inachukua nusu ya eneo la hifadhi. Maeneo ya uwanda wa chini yenye misitu michache na yaliyoathiriwa na ukataji miti, uchomaji moto ni asilimia 6 ya eneo lote. Asilimia 6 nyingine za eneo la chini ya milima zimeingiliwa na spishi za miti za kutoka nje ya hifadhi kama vile Maesoppsis eminii, Cedrella odorata na michikichiki. Baadhi ya miti hii migeni iliingia kupitia bustani ya mimea ya Amani ambayo ilianzishwa kuhifadhi mimea ya Afrika. Katika Hifadhi ya Asili ya Amani, mimea isiyo ya misitu ni michache sana, ikiwa katika ardhi kavu za vichaka (2%), ardhi ya nyasi, maeneo ya miamba na mabwawa na mito (yote yakiwa na chini ya 1%).

## *Muundo wa Uongozi*

Hifadhi inamilikiwa na serikali kuu ya Tanzania kupitia Kitengo cha Misitu na Ufugaji wa Nyuki cha Wizara ya Maliasili na Utalii lakini usimamizi wa kila siku wa hifadhi unafanywa na Mhifadhi. Mhifadhi anatarajiwa kuyajadili mambo muhimu yahusuyo hifadhi na Bodi ya Ushauri, ambayo, kimsingi, hukutana mara mbili kila mwaka au kulingana na mahitaji. Majukumu yake ni pamoja na kuidhinisha bajeti na mpangokazi wa hifadhi. Bodi hiyo huundwa na wawakilishi wa wadau mbalimbali, zikiwemo jamii za wenyeji, mamlaka za mkoa na wilaya, na asasi nyingine kama vile Kampuni ya Chai na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania.

Uhusishwaji wa jamii za wenyeji umekuwa ni sehemu muhimu katika mafanikio ya Hifadhi ya Asili ya Amani tangu kuanzishwa kwake. Njia ya Tathmini shirikishi inayofanywa na vijiji ilitumiwa kufanya mipango ya mipaka baina ya vijiji. Kabla ya hapo, serikali ya Tanzania ilikuwa imetumia mbinu kama hizo kuwahusisha wenyeji katika usimamizi wa msitu, uanzishaji wa Hifadhi za Misitu ya Vijiji na maeneo ya usimamizi wa pamoja wa misitu katika hifadhi za serikali, ambako rasilimali za misitu zilikuwa zikisimamiwa kwa pamoja na Kitengo cha misitu na nyuki cha serikali. Mipango ya vijiji ya usimamizi wa rasilimali imeandaliwa na jamii za wenyeji kwa ajili ya usimamizi endelevu zaidi wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya mipaka ya hifadhi na kupunguza madhara ya binadamu kwa msitu. Watu wawili huwakilisha jamii za wenyeji kwenye bodi ya ushauri ya hifadhi ya asili ya amani – mmoja kutoka katika katika kila wilaya inayopakana na hifadhi, Korogwe na Muheza. Wawakiklishi wa jamii za wenyeji huchaguliwa na vijiji vyao.

## *Kuyatimiza mahitaji ya kimaisha ya wakazi wa eneo la hifadhi*

Mpaka wa hifadhi wenye urefu wa kilometa 149 unajumuisha vijiji kadhaa na nyumba zilizotawanyika. Kilimo cha kibiashara na chakula ndiyo shughuli muhimu ya jamii za wenyeji katika mipaka ya Hifadhi ya Asili ya Amani, kukiwa na mashamba yenye wastani wa hekta 2.7. Mazao makuu ya chakula ni mahindi, mihogo, ndizi na maharage. Mazao makuu ya biashara ni mahindi, miwa, iliki, mdalasini, karafuu, na pilipili nyeusi. Sehemu kubwa ya ardhi ya kijiji ipo chini ya mfumo wa kimila wa umiliki lakini ardhi huazimwa na kununuliwa pia. Njia zisizo endelevu za kilimo zilisababisha uharibifu wa udongo na kupunguza uzalishaji wa kilimo; matumizi ya matungazi, na mbolea ya asili havikuwepo sana miaka ya 1990. Kukosekana kwa eneo linalofaa kwa kilimo ndiyo chanzo kikuu cha uharibifu wa mfumo wa ikolojia, ikichangiwa na kutokuwepo kwa vyanzo mbadala vya kipato.

Ustawi wa jamii za wenyeji ni jambo la muhimu kwa mafanikio ya hifadhi, kwa kutumia mfumo wa kugawana mapato na miradi mbalimbali ya njia mbadala za kuendesha maisha kwa manufaa ya vijiji hivi. Hifadhi ya Asili ya Amani imegawanywa katika kanda mbalimbali zenye hadhi tofauti za uhifadhi: kanda ya uhifadhi wa bayoanuwai inachukua hadi 77% ya eneo, wakati kanda ya matumizi ya wenyeji ni 6% ya eneo hilo. Kanda ya mpaka ilianzishwa pia kwa ajili ya kudumisha njia endelevu za matumizi ya rasilimali na kupunguza utegemezi wa jamii za wenyeji kwenye maliasili za Hifadhi ya Asili ya Amani na kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya jamii hizi, kwa kuzihusisha katika usimamizi wa Hifadhi ya Asili ya Amani (Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Hifadhi ya Asili ya Amani, 1998). Ushirika baina ya jamii za wenyeji unaelezwa katika sheria za matumizi ya makubaliano ya mgawanyo wa mapato. Wanajamii wanaruhusiwa kukusanya kuni katika kanda ya matumizi ya wenyeji mara mbili kwa juma na kukusanya mimea ya tiba kwa ruhusa maalumu. Kwa ajili ya kufidia udhibiti huu, vijiji vya mpakani vinapata 20% ya ada za kiingilio na utafiti katika hifadhi ya asili.



# **Majukumu Makuu** na Ubunifu



Utegemezi mkubwa wa jamii za wenyeji katika maliasili zilizopo katika eneo hili ulikuwa ndiyo kichocheo kikubwa cha mradi. Hifadhi inatumia mbinu za kuendeleza njia mbadala za kuijpatia kipato kama vile utalii wa mazingira, ufugaji wa nyuki, samaki na vipepeo, kilimo cha matunda na vitalu vya miti. Baadhi ya program hizi zimejaribu kuunganisha maarifa ya jadi na mifumo ya kisasa ya uzalishaji.

## *Njia endelevu za kuboresha maisha*

Utalii wa Mazingira: Utalii wa mazingira umekuwa chanzo kikuu cha mapato kwa jamii za hifadhi hii ya asili, na fedha zinawekezwa tena katika shughuli za uhifadhi. Hifadhi hii ya asili ina njia za watembea kwa miguu msituni, matembezi ya usiku, kambi, ziara katika mashamba ya vipepeo na kutazama ndege. Shughuli hii ya mwisho imekuwa maarufu sana, na watazamaji wengi wa ndege wanaotmbelea Amani wana matarajio ya kuzitambua aina 340 za ndege Usambara Mashariki. Hii ni pamoja na ndege walioko hatarini kutoweka kama vile Bundi Kusi (Bubo vosseleri), Usambara Weaver (Ploceus nicolli), Amani Sunbird (Anthreptes pallidigaster), na Long-billed Tailorbird (Orthotomus moreaui).

Mradi wa vipepeo wa Amani: Njia nyingine mbadala ya kuendesha maisha ni ufugaji wa vipepeo. Amani ina ushirikiano na shirika la madawa la ulaya ambalo hununua vipepeo wachanga, na kuwa chanzo kikubwa cha kipato kwa wakulima wenyeji. Kadhalika, katika ufugaji wa nyuki, ujuzi wa jadi umeunganishwa na mifumo ya kisasa ili kuwezesha kuwepo kwa mashamba ya nyuki binafsi na ya pamoja kwa ajili ya uzalishaji wa asali.mifumo ya kijadi ya ukusanyaji wa kaa kutoka katika mito na ardhi  imeunganishwa na njia za kiasasa za ufugaji wa samaki kwa ajili ya biashara na chakula. Shughuli hizi zimeanzishwa zikiwa na viwango mbalimbali vya mafanikio kupunguza athari za binadamu kwa mfumo wa ikolojia ya msitu, pasipo kuharibu bayoanuwai ya hifadhi.

Kilimo cha uyoga; majiko ya nishati kidogo: Katika sehemu ambazo vikundi vya wanawake vimekuwa vikikusanya mboga za majani katika maeneo makuu ya bayoanuwai ya hifadhi, mafunzo yametolewa ili kuendesha bustani nje ya maeneo ya bayoanuwai, ikiwa ni pamoja na kilimo cha uyoga. Kadhalika, mahali ambapo jamii za wenyeji zilitegemea zaidi kuni kutoka katika hifadhi, na wanawake wakiwa na kazi kubwa zaidi, majiko ya nishati kidogo yametolewa kwa vijiji vyote na jamii za maeneo ya karibu na Hifadhi ya Asili ya Amani.

Kilimo cha Misitu na Urejeshaji wa Miti iliyokatwa: Amani inajihusisha na shughuli za kilimo cha misitu katika maeneo ya mpaka wa hifadhi ili kuweka mfumo endelevu wa usimamizi wa mazao ya  misitu na kupunguza utegemezi wa wenyeji kwa bayoanuwai ya hifadhi. Mipango ya vijiji ya usimamizi wa maliasili imeendelezwa ikizihusisha jamii za wenyeji na vijiji katika maamuzi ya matumizi ya rasilimali. Katika shughuli zote za kilimo cha misitu na urejeshaji wa misitu, spishi za miti zinachaguliwa kwa makubaliano kwa kushauriana na jamii za wenyeji. Shughuli hizi zimejikita katika kupanda spishi za kienyeji na kuzuia kusambaa kwa spishi za kigeni.

Uhifadhi wa udongo: Njia za uboreshaji wa matumizi ya ardhi na uhifadhi wa udongo zimeboreshwa pia. Katika kanda za mipaka ya hifadhi, kuna ardhi kubwa iliyopumzishwa ambayo haifai tena kwa uzalishaji wa iliki, miwa, ndizi au mahindi. Hata hivyo, ardhi hii inafaa kwa kilimo cha pilipili nyeusi na karafuu. Soko la ndani la mazao haya linaendelea kukua. Jamii za wenyeji zinasaidiwa kuhamia kwenye kilimo cha pilipili nyeusi na karafuu, mazao ambayo, mbali na kujiongezea kipato, yamethibitika kuwa na manufaa katika uhifadhi wa udongo na kupambana na mmomonyoko. Mafunzo ya usimamizi na mafunzo mengine ya kujenga uwezo hutolewa kwa jamii za wenyeji, ambao wanawakilishwa pia kwenye Bodi ya Ushauri. Jamii za wenyeji hushiriki katika shughuli za Amani na usimamizi kupitia mikutano, warsha, nafasi za kazi na mawasiliano ya kila siku.

# Matokeo



## MATOKEO YA KIMAZINGIRA

Ndani ya hifadhi, kuna idadi kubwa ya spishi za wanyama na mimea isiyopatikana sehemu nyingine. Uhifadhi wake unategemea kupungua kwa shinikizo la shughuli za kibinadamu katika mifumo ya hifadhi ya mazingira; Hifadhi ya Asili ya Amani imefanikiwa kupunguza shinikizo hizo kwa kuendeleza njia mbadala za maisha kwa kugawanya mapato yanayotokana na utalii wa mazingira na kusimamia utalii wa mazingira na kuweka sheria za matumizi ya ardhi.

### *Uwekaji wa kanda za mazingira na urejeshaji wa msitu*

Matumizi ya ardhi katika hifadhi ya asili yamegawanyika katika kanda nne. Eneo la hifadhi ya bayoanuwai ambayo ndiyo sehemu kubwa ya Amani, ikiwa na asilimia 77 ya eneo lote. Asilimia 13 ya eneo limetengwa kwa ajili ya kurejesha uoto wa asili, ambako upandaji wa miti ya kienyeji hufanywa ili kuurejesha msitu uliopotea kutokana na ukataji haramu wa miti. Eneo la matumizi ya wenyeji ni asilimia 6 ya eneo lote wakati bustani ya mimea ya Amani inachukua asilimia 4 ya hifadhi.

Mipaka ya eneo la hifadhi imewekwa wazi na wanajamii wamejitolea kufanya doria ili kudhibiti shughuli haramu za kibinadamu. Katika miaka ya karibuni, shughuli hizi zimehusisha ukataji magogo, uwindaji haramu, uchimbaji wa dhahabu na kutoa magome ya mkwinini kwa ajili ya uzalishaji wa dawa ya kwinini. Tangu kuanzishwa kwa hifadhi hii, shughuli hizi haramu zimepungua sana na pia uchomaji moto na uwindaji haramu.

Maeneo yaliyokuwa yameharibiwa kwa moto yanarejeshwa na misitu iliyopotea kutokana na ukataji magogo inapandwa tena kila mwaka kwa kutumia spishi za miti na mimea ya kienyeji. Aina mbalimbali za spishi za kienyeji hutumika ili kuepuka kuwepo kwa aina moja ya miti. Hifadhi ya Asili ya Amani imelenga kupunguza idadi ya spishi za kigeni na kusaidia kurejesha uoto wa kienyeji. Spishi ya *Psidium cattleyanum* imepangwa kuondolewa wakati *Cedrela odorata* na *Melia azedarach* imepunguzwa. Usimamizi wa mara kwa mara wa *Maesopis eminii* hufanywa, ingawa hakujwa na shughuli zinazofanywa kuiondoa spishi hii.

Majadiliano yamekuwa yakiendelea tangu mwaka 2000 ili kulichukua eneo derema ambalo halimo katika hifadhi ili kulifanya liwe Hifadhi mpya ya Asili chini ya serikali kuu. Eneo hili muhimu la msitu huiunganisha sehemu ya kusini ya Hifadhi ya Amani na hifadhi nyingine za misitu za kitaifa zilizopo kaskazini mwa Usambara Mashariki. Uhifadhi wa msitu huu ni muhimu kwa ajili ya uendelevu wa kiikolojia wa maeneo yote mawili.

### *Uhifadhi wa viumbe vilivyo katika hatari ya kupotea*

Milima ya Mashariki ya Usambara imejumuishwa katika 'jamii inayohatarishwa kutoweka' katika kitabu chekundu cha data za viumbe wasio na uti wa mgongo cha IUCN. Spishi nyingi zisizo na uti wa mgongo za milima ya usambara mashariki hazipatikani sehemu nyingine. Kwa mfano, spishi 41 za jongoo zimebainishwa na 85% ya spishi hizi hazipatikani sehemu nyingine. 45% ya konokono wa chi kavu waliopo ndani ya hifadhi hawapatikani sehemu nyingine wakati konokono wa aina ya Gulella ni 75%. Spishi 15 katika ya 37 za vipepeo wa misitu ya milimani, Mashariki mwa Usambara pia hazipatikani mahali pengine.

Pia Hifadhi ya Asili ya Amani ni makazi ya spishi za wanyama wakubwa. Spishi kumi na tano za vyura wa msituni na spishi kumi na tatu za reptilia zilizopo Mashariki mwa Usambara hazipatikani sehemu nyingine Tanzania. Kadhalika, spishi nyingine za mamalia zimeorodheshwa kidunia kama viumbe viliyopo katika hatari ya kutoweka - popo (*Myonycteris relicta*), nguchiro kijivu (*Bdeogale crassicauda*), Mindi (*Cephalophus spadix*), Panya-buku (*Rhyncochyon petersi*) - wakati spishi nyingine ndogo, Perere (*Dendrohyrax*

*validus vosseleri*)zinaweza kuwa hazipatikani sehemu nyingine. Mamalia wanaopatikana kwa wingi ni wale wa jamii ya nyani: Nyani (*Cercopithecus mitis*), Nyani aitwaye Colubus (*Colubus guereza*) na Ngedere wa Njano (*Papio cynocephalus*).

Baraza la Kimataifa la Uhifadhi wa Ndege (ICBP) imeitaja misitu iliyopo chini ya milima na ile ya uwanda wa chini wa Usambara Mashariki kuwa Maeneo ya Ndege Wasiopatikana sehemu nyingine. Kuna spishi kumi na tatu zilizopo katika hatari ya kutoweka kidunia ambazo nyingi ya hizo hazipatikani sehemu nyingine au katika misitu mingine ya Usambara Mashariki. Misitu ya Usambara Mashariki imetambuliwa kuwa kati ya maeneo matatu Afrika yenye ndege wasiopatikana sehemu nyingine na kama eneo muhimu kabisa ya sehemu ya nchi kavu ya Afrika kwa kuwa na ndege wanaotishwa kutoweka duniani. Spishi hizi ni pamoja na kolokolo (*Apalis moreaui moreaui*), bundi kusi (*Bubo vosseleri*), Chozi wa Amani (*Anthreptes pallidigaster*), Kwera wa Milima ya Usambara (*Ploceus nicolli*) na Swnnerton's Robin (*Swynnertonia swynnertoni*).

3.1% ya mimea iliyopo katika hifadhi inapatikana katika milima ya Usambara Mashariki pekee, kwa kujumuisha spishi ambazo zinakaribia kuwa na sifa hizo au zile zilizopo karibu na Milima ya Usambara Mashariki, inafikia 22%. Spishi 1,921 za mimea yenye neli zimeripotiwa kuwepo Usambara Mashariki. Hii inajumuisha spishi 64 za mimea isiyopatikana sehemu nyingine au inayokaribia kuwa na sifa hiyo. Kati ya spishi zinazojulikana zisizopatikana sehemu nyingine ni pamoja na aina ishirini za maua ya urujuani ya Afrika (*Saintpaulia spp*), ambapo moja ya spishi hizo ilipelekwa kwa mara ya kwanza Ulaya na Kamishna wa Kijerumani, Tanga mwaka 1891. Spishi nyingine zilizotambuliwa ambazo hazipatikani sehemu nyingine au ambazo zinakaribia kuwa na sifa hiyo zilizopo Hifadhi ya Asili ya Amani ni *Leptonychia usambarensis*, *Cephalosphaera usambarensis*, na *Allanblackia stuhlmannii*.

# MATOKEO YA KIJAMII

Jamii za wenyeji katika kanda za mipaka ya Hifadhi ya Amani zinapokea asilimia 20 ya mapato ambayo ni Dola za Kimarekani 4,000 kwa mwaka. Makubaliano haya yamezingatia malengo ya hifadhi hii ya asili na imeziwezesha jamii kuwekeza fedha zao katika miradi ya maendeleo. Mbali na muundo wa kugawana mapato katika hifadhi, njia mbadala za kuendesha maisha zinafanywa na jamii mbalimbali.

## *Kuongeza vyanzo vya kipato*

Wakulima wanaoishi karibu na mipaka ya hifadhi wamesaidiwa kupanda zaidi ya miti 10,000 ambayo inatoa nishati ya kuni, vifaa vya ujenzi, na fursa za kipato cha NTFP kwa wakulima. Mpango mmopjwapo uliofanikiwa ulihusisha uuzaji wa mafuta ya mimea ya allanblackia. Mimea hii hupatikana katika kituo cha Amani ambacho ikiwa na matunda makubwa hadi kufikia nchi 12 ambayo inaweza kuwa na mbegu 40-50.karnel hiyo huzalisha fati ngumu nyeupe ambayo inaweza kubanguliwa na kutumika kama sabuni au kupikia. Kituo cha Amani kimejikita katika kuchambua aina za udongo kwa ajili ya kuzalisha *allanblackia*, na miche 12,500 imetolewa kwa wanavijiji katika vijiji 19 kwa ajili ya kupanda katika vitalu vya bustani. Kituo cha Kimataifa cha Kilimo cha Misitu (ICRAF), Shirika la Kimataifa la Maendeleo (IUCN), na Asasi ya Maendeleo ya Uholanzi (SNV) vimeshirikiana na Unilever na asasi za ndani ya nchi, ikiwemo Novel Development Tanzania Ltd (NDTL) na Kikundi cha Uhifadhi wa Misitu Tanzania (TFCG) kuendeleza uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko kwa ajili ya usindikaji wa mafuta ya *allanblackia*.

Zaidi ya watu 4000 wameajiriwa kupitia shughuli za ufugaji wa nyuki na vipepeo. Chama cha ushirika cha wafugaji wa vipepeo kimeanzishwa kwa ajili ya kuzalisha na kuuza vipepeo nje ya nchi.





Buu wa vipepeo huuzwa kwa kati ya Dola ya Kimarekani 1 na 2.50. Kwa wastani, mradi wa ufugaji wa vipepeo umeongeza kipato cha familia kwa kiasi cha asilimia 25, ikiwahamasisha wakulima kulinda misitu inayowazunguka.

Kwa msaada wa uongozi wa hifadhi, wakulima wengi sasa wanapata kipato kinachotokana na kuboreshwa kwa uzalishaji wa asali. Mradi wa Amani unawapa wakulima mizinga ya kisasa, ambayo inaboresha shughuli za asili za ufugaji wa nyuki. Misaada hutolewa kwa ajili ya ufugaji wa nyuki na usindikaji wa asali. Uongezaji wa shughuli za kilimo unatolewa kwa kuwasaidia wakulima katika uvunaji wa karafuu, iliki, mdalasini, miwa, viazi vikuu na pilipili nyeusi (mazao ya biashara), na mihogo, viazi vikuu na ndizi (mazao ya chakula). Shughuli za ufugaji wa wanyama huendelezwa pia. Uzalishaji wa maziwa umeanzishwa katika eneo hii kupitia sera ya 'Ufugaji wa Ndani' (*Zero Grazing*), ambao ni chanzo kikubwa cha mapato (pamoja na mboji inayohitajika kwa ajili ya kuongeza rutuba katika ardhi).

Ufugaji wa kaa na samaki umeendelezwa kwa ajili ya matumizi ya kiabiashara na ya chakula. Kwa kuyatambua madhara ya mabwawa ya samaki kwa ardhi oevu na ubora wa maji, Mradi wa Amani ulisaidia ujenzi wa mabwawa ya kisasa tu. Maeneo ambayo kumekuwa na ukataji wa fito kwa ajili ya kuundaa mashamba, vikundi vya wenyeji vimesaidiwa kuibadilisha kazi ya jamii kuelekea uzalishaji wa matofali ya udongo wa mfinyanzi kwa ajili ya kujenga nyumba zinazodumu zaidi na za kisasa.

### *Manufaa yanayotokana na uboreshaji wa ustawi wa jamii za wenyeji na vyanzo vya maji*

Vijiji tisa vimeanza kutumia majiko bora ya kuni na kujenga nyumba kwa kutumia matofali ya kuchoma. Majiko yanayotumia nishati kidogo na yanayoweza kupunguza matumizi ya nishati katika kaya kwa asilimian 50 ikilinganishwa na 'majiko ya zamani ya mafiga matatu'- yamefanikiwa kupunguza matumizi ya misitu. Majiko haya pia yamekuwa na manufaa ya kiafya kwa jamii za wenyeji kwa kupunguza uvutaji wa moshi na magonjwa ya mfumo wa upumuaji. Hifadhi ya Asili ya Amani ni moja ya vyanzo vya maji katika eneo la mashariki mwa milima ya Usambara. Mto Zigi ni chanzo cha maji kwa mji wa Tanga na jamii za jirani. Hifadhi ya Amani hutoa pia maji kwa ajili ya vituo vya nishati ya maji vya Hale na Pangani kupitia mto Pangani wakati sehemu ya Magharibi humwaga maji yake katika Bonde la Lwengera.

## MATOKEO YA KISERA

Ikiwa kama hifadhi inayoendeshwa na serikali, Amani imekuwa mfano wa usimamizi wa mistu Tanzania na mfano wa uhifadhi wa bayoanuwai kidunia.

Mabadiliko ya sera na sheria Tanzania kwa miaka michache iliyopita yameonyesha kwamba msingi wa kuzihusisha jamii za wenyeji katika uhifadhi wa msitu, usimamizi wa msitu na urejeshaji wa msitu umeshawekwa. Sheria ya ardhi ya Tanzania (1999) inatambua haki za jamii za wenyeji kulipwa fidia kwa ajili ya ardhi ambayo wanakubaliana kuitenga kwa ajili ya hifadhi, mbinu ambayo imeigwa na Hifadhi ya Asili ya Amani. Hii inaendana na Sera ya Misitu ya Taifa (1998) na Sheria ya Misitu (2002), na inaweza kuonekana katika jitihada mbalmbali za kuitumia mahali pengine, ikiwemo Hifadhi ya Msitu wa Derema ambayo inapakana na Amani upande wa Kaskazini.

Kutokana na jitihada za Hifadhi ya Asili ya Amani, milima ya Usambara Mashariki iliweza kuingizwa katika Programu ya Hifadhi ya Binadamu na Mazingira ya UNESCO. Misitu ya Milima ya Mashariki ilitangazwa kuwa Eneo la Urithi wa Dunia mwaka 1997 kwa kutambua thamani yake ya asili kidunia, ingawa hadhi hii iliondolewa na Serikali ya Tanzania Machi 2011. Misitu ya Amani imetambuliwa na mashirika mengine ya kimataifa kama vituo muhimu vya kimataifa vya bayoanuwai ikiwemo Shirika la Mazingira Duniani (IUCN), Mfuko wa Dunia wa Wanyamapori na Baraza la Dunia la Uhifadhi wa Ndege.

# Jinsi ya Kudumisha Mradi Huu



## JINSI YA KUDUMISHA MRADI HUU

Hifadhi ya Asili ya Amani imeanzisha mfuko wa hifadhi kwa ajili ya gharama za uendeshaji. Mapato yanayotokana na utalii yanachangia kwenye mfuko huu lakini hayagharamii maeneo yote ya progarmu ya hifadhi. Hii inategemea vyanzo vya fedha vya nje. Kwa hiyo, kwa msaada wa fedha zinzotolewa kwa nyakati mabalimbali kama vile Programu ya Misaada Midogo ya Shirika la UNDP, au Mfuko wa Critical Ecosystems Partnership Fund. Uendelevu wa msaada kutoka nje ni muhimu kwa aijili kuendeleza usimamizi wa misitu ya hifadhi hii ya asili.

Kadhalika, vitisho kwa uendelevu wa kimazingira wa Hifadhi ya Amani vimebainishwa.Hii ni pamoja na kujitenga na mfumo wa ikolojia wa Usambara Mashariki. Mbinu ya kukabiliana na tatizo hili ni kuutangaza Msitu wa Derema kuwa Hifadhi ya Msitu ya Serikali kuu. Matatizo yanayohusiana na rasilimali za kifedha yanaweza kuwa na athari kwenye mapato ambayo yanachangiwa na jamii za mipakani, ambayo hutumika kama njia kuu ya fidia kwa ajili ya udhibiti wa kuzitumia rasilimali za msitu.

Miundombinu hafifu imebainishwa kuwa udhaifu wa hifadhi hii ya asili. Hoteli kubwa inafikiwa kwa safari ya kilometa 35 kutoka barabara kuu. Pia miundombinu ya malazi kwa watalii haitoshelezi na kuna ukosefu wa mipangilio ya shughuli za kufanywa na wageni. Mwisho, kuwapo kwa uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu unaochangiwa na tetesi za kuwepo kwa madini katika mito, uchomaji moto misitu vienaendelea kuwa tishio kwa msitu.

## MAONO

Hifadhi ya Asili ya Amani ilitumika kama mfano wa kuigwa na hifadhi nyingine Tanzania. Mfumo huu wa usimamizi umetumiwa pia katika hifadhi za asili saba za Milima ya Mashariki. Hadhi ya Hifadhi ya Asili ni ya kiwango cha juu kabisa cha udhibiti chini ya sheria za Kitengo cha Ufugaji wa nyuki na ni sawa na hadhi ya Mbuga za Wanyama za Taifa zilizoko chini ya Mamlaka ya Mbuga za Wanyama za Taifa.

Hifadhi ya Asili ya Kilombero ilitangazwa mwezi Agusti 2007, ikiziunganisha Hifadhi tatu za zamani za Misitu katika Milima ya Udzungwa iliyopo eneo la Kusini-Kati mwa Tanzania. Msaada kwa ajili ya Kitengo cha Misitu na Nyuki kuitangaza hifadhi hiyo ulitolewa na shirika la Miundombinu ya Mazingira Duniani (Global Enviromental Facility), mtandao wa WWF, na Mfuko wa Critical Ecosystem Partnership Fund. Hifadhi hii  ina safu ya milima yenye mita 300-2,600 na inajumuisha misitu, maeneo makubwa ya ardhi ya nyasi na ardhi oevu katika maeneo ya miinuko. Jumla ya spishi zake inaifanya Kilombero kuwa eneo muhimu kabisa la uhifadhi la Milima ya Mashariki.

Muda mfupi baadaye, Hifadhi nyingine mbili za Asili zilianzishwa kwenye Milima ya Mashariki. Hifadhi za misitu za Ulugulu Kaskazini na Ulugulu Kusini ziliunganishwa na kuunda Hifadhi ya Asili ya Uluhulu ambayo ilianzishwa kulinda vichaka vya ulugulu vilivyoko hatarini kupotea. Hifadhi ya Msitu wa Nilo iliyopo Mashariki mwa Milima ya Usambara ilipandishwa pia ilipandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Asili. Hivi karibuni, Hifadhi za Asili zimeanzishwa sehemu zote za Milima ya Mashariki, Shune, Magamba, Chome, Rugwe na Nkingu. Uchambuzi wa awali wa kiuchmi wa mfumo wa ikolojia unaonyesha kwamba Milima ya Mashariki huchangia kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 620 kwenye uchumi wa Taifa kwa mwaka, bila kuzingatia kikamilifu thamani ya maji utalii na huduma za mazingira.

## WAHISANI


Kitengo cha Ufugaji wa Nyuki cha Wizara ya Maliasili na Utalii, Serikali ya Tanzania


- Kikosi cha Hifadhi ya Misitu Tanzania (TFCG)
- UNDP/GEF Small Grants Program: Small Grant Recipient 2003-4, 2004-6
- Critical Ecosystem Partnership Fund


# MAREJELEO YA ZIADA


- Amani Nature Reserve Photostory [EN] http://vimeo.com/15783369 [Swahili] http://vimeo.com/15783445
- Amani Butterfly Project Website http://www.amanibutterflyproject.org
- Milledge, S. and Elibariki, R. 2004. *Green Gold: Ongoing efforts towards preventing illegal harvesting and exports of Tanzania's most valuable hardwoods*. The Arc Journal. Download here.
- Morgan-Brown, T. 2007. *Butterfly Farming and Conservation behavior in the East Usambara Mountains of Tanzania*. Master's Thesis, University of Florida. Download here.


*Masimulizi kuhusu miradi mingine, bonyeza hapa:*





Equator Initiative
Environment and Energy Group
United Nations Development Programme (UNDP)
304 East 45th Street, 6th Floor
New York, NY 10017
Tel: +1 646 781-4023
www.equatorinitiative.org


EQUATOR INITIATIVE

Mradi wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa ndio unaoendesha miradi ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa kote ulimwenguni kwa kutoa mwito wa mageuzi na kuelekeza mataifa kwa maarifa, na malighafi ili kusaidia watu kujiimarisha kimaisha.

Mradi huu wa Equator huleta pamoja Umoja wa Mataifa , serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, wafanyibiashara na makundi ya mashinani ili kutambua na kuimaliza maendeleo himili kwa watu na jamii kwa jumla.


©2012 Haki Zote ni za Mradi wa Equator